



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**KUHUSU UAMUZI WA RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA MSIMAMIZI MSAIDIZI
WA UCHAGUZI WA KUTOWATEUA WAGOMBEA WA UDIWANI KATIKA
KATA YA BWONGERA, HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO,**

MKOA WA GEITA

Dodoma, Tarehe 18 Mei, 2026

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 65(7) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea rufaa tano (05) za wagombea Udiwani wanaopinga uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata ya Bwongera wa kutowateua kuwa wagombea.

Katika kikao chake maalum kilichofanyika tarehe 15 Mei, 2026, Tume ilisikiliza na kuzikubali rufaa (02). Rufaa tatu (03) zilizokuwa zimebaki zimesikilizwa na Tume katika kikao chake cha leo tarehe 18 Mei, 2026 ambapo imezikubali rufaa zote tatu (03) kama ifuatavyo: -

- i. **Ndugu Magreth Lucas Masasi** mgombea Udiwani kupitia Chama cha MAKINI dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Bwongera;
- ii. **Ndugu Zena Hamad Said** mgombea Udiwani kupitia Chama cha TLP dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Bwongera; na
- iii. **Ndugu Hanifa Sembe Mohamed** mgombea Udiwani kupitia Chama cha UMD dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Bwongera.

Hivyo, wagombea tajwa, wamerejeshwa katika orodha ya wagombea Udiwani katika kata husika na waendeleo na taratibu za kampeni za uchaguzi mdogo wa Udiwani utakaofanyika tarehe 01 Juni, 2026.

Imetolewa na:

Kailima, R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

